



SWAFAR 1448 HIJIRIA - AGOSTI 2026 MILADIA (Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO

MIKA 30 YA 'BONGO FLAVA: MIKA YA UHARIBIFU KWA VIJANA



Tarehe 10 Julai 2026, tamasha la "Miaka 30 ya Bongo Flava" lilizinduliwa jijini Dar es Salaam kuadhimisha miaka 30 tangu kuzaliwa kwa muziki wa Bongo Flava. Muziki huu ulianza kama mchanganyiko wa muziki wa Hip-Hop wa Marekani, mitindo ya muziki wa asili wa Tanzania na simulizi za lugha ya Kiswahili. Maadhimisho hayo yanalenga kuwatambua na kuwaheshimu wasanii pamoja na watu mbalimbali waliochangia kuukua na kuufanya muziki huo kuwa maarufu.

Muziki wa Bongo Flava uliibuka kuwa natija ya uvamizi wa kitamaduni kutoka kwa Wamagharibi kwa kuiga muziki wa hip-hop wa Marekani. Mabepari Wamagharibi Makafiri hawakuridhika tu na ukoloni na ukoloni mamboleo katika nyanja za siasa na uchumi wa nchi, bali pia walitumia

mashambulizi ya kitamaduni kama njia ya kuwalaza akili vijana na kuifanya jamii itawaliwe kiakili kwa kuwa na ndoto zisizo na uhalisia na matumaini hewa kupitia aina mbalimbali za burudani, ikiwemo Bongo Flava.

Bongo Flava iliibuka nchini Tanzania kutokana na kuiga muziki wa hip-hop ya Marekani kwa Kiswahili. ilifuata kwa kiwango kikubwa mwelekeo na ushawishi wa hip-hop ya Marekani, kama ambavyo muziki wa hip-hop ulivyoathiri na kuharibu maadili ya vijana wa Marekani ndivyo ambavyo Bongo Flava imeharibu vijana wa Tanzania.

Kwa miongo mitatu, Bongo Flava imetumika kueneza ufuska na maadili ya Kimagharibi na kukuza vitendo yanayovunja maadili ya jamii, kama vile uzinzi, ulevi na mapenzi ya jinsia moja (LGBTQ). Mambo ambayo ni hatari katika kusambaratisha maadili ya jamii.

Matokeo yake wasanii
Inaendelea ...Uk. 3

KATIBA ZA KUTUNGWA NA BINADAMU

Katiba za kibinadamu licha ya kuwa ni haramu moja kwa moja Kiislamu kwa kuwa ziko kinyume na Uislamu. Bali kwa udhati wake pia zina mapungufu makubwa na zinapingana hata na akili ya mwanaadamu lau mwanadamu huyo atakua mchambuzi na mwerevu kidogo tu. Kama tutakavyoonesha mbele InshaAllah.

Katiba ambayo ndiyo sheria mama kwayo sheria nyengine zote hutokamana nayo, kwa sifa yake ya msingi na maumbile yake ni sheria kama zilivyo sheria nyengine. Na tunaposema katiba za kidemokrasia hazikubaliani hata na akili maana yake kila sheria inayozilikana kutokana na katiba hiyo pia huwa haifai na ingongana na akili. Kwa kuwa ikiwa katiba ambayo ni sheria mama ni batil humaanisha kila kinachozalikana na sheria hiyo huwa nacho batil.

Miongoni mwa dalili za kiakili kwamba katiba za kibinaadamu hazina mashiko na hazikubaliani na hata akili ni kama zifuatazo:

1. Wanaadamu hawawezi kukubaliana.

Inaendelea Uk. 3

Yaliyomo :

- ♦ **Vijana na Mabadiliko ya Kiislamu.....2**
- ♦ **Mali Iliyoporwa.....4**
- ♦ **Ndoa haitenganishwi na Khilafah.....5**
- ♦ **Kuwaandaa wanawake kwa Daawa 7**

VIJANA JIUNGENI KWENYE MABADILIKO YA KWELI YA KIISLAMU.

Tarehe 12 Agosti ya kila mwaka imechaguliwa kuwa Siku ya Vijana Kimataifa. Mabepari hudai kwamba siku hii ni muda wa kutafakari na kuanisha changamoto mbali mbali za vijana na kuleta ufumbuzi.

Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2015 za Shirika la Umoja wa Mataifa la Ajira (ILO) asilimia 25% tu ya waajiriwa duniani ndio vijana. Hii inamaanisha wengi wa waajiriwa ni watu waliovuka umri wa ujana, ilhali zaidi ya asilimia 43% ya vijana duniani hawana ajira. Katika nchi zinazoendelea ambazo ni makoloni ya mataifa kibepari ya kimagharibi asilimia 31% ya vijana wake amma hawana elimu ya kujitosheleza kuweza kuajiriwa au hawana ajira licha ya elimu yao. Tunaweza kusema hali ya vijana kiulimwengu ni mbaya sana, na wengi wao wamekosa matumaini ya kuishi kamwe! Mfumo kandamizi wa kibepari umewatelekeza vijana kiasi cha kufikia wengine kuchukua maamuzi magumu ambayo hayafai kama kujiua, matumizi ya madawa ya kulevya nk.

Tokea zama za dahari vijana wamekuwa wakiwindwa ili kutumika kwa mbinu mbalimbali kama vile kuwatia tamaa na matarajio ya uongo pamoja na ahadi zenye matumaini wasiyotekelezewa daima. Haya hufanywa makusudi tena zaidi na wanasiasa na wanaharakati wakijua na kuamini kwamba watakapoungwa mkono na vijana, wakiweza kuwadhibiti na kushikilia fikra zao basi itakuwa



wamejiwekea mkakati muhimu sana kwao katika kuondosha au kupunguza hatari na tishio kwao.

Ujana ambao ni hidaya adhimu na amana kwa mwanadamu leo inatumika kwa maslahi ya mfumo batil wa kibepari. Ni katika wakati huu wa ujana ambapo mwanadamu huwa na uwezo mkubwa wa nguvu za kiwiliwili na uwezo mkubwa wa kiakili wa kujenga hoja na tafakuri. Ujana hufananishwa na jua la mchana lingaapo, na uzee huchukuliwa kama jua lituapo ukihusishwa na udhaifu. Mambo mengi ama ya faida au ya hasara hafanyika wakati wa ujana, wanavyuoni wengi waliitafuta na kupata elimu yao katika umri wa ujana. Kwa mfano, mwanachuoni, mwanasiasa na mujtahidi mkubwa wa zama hizi sheikh Taqiuddin An-Nabahan (Allah Amrehemu) alikuwa tayari ameshahifadhi quran yote akiwa tu kijana wa miaka 12.

Wimbi kubwa mabadiliko haramu ya mfumo batil wa kidemokrasia huungwa mkono moja kwa moja na vijana. Tena kwa masikitiko baadhi yao wengi ni vijana wa Kiislamu. Vijana hao hushiriki katika michakato hiyo kwa ujasiri, ushupavu, mihanga mkubwa na moyo wa kufa na kupona katika kuona kwamba ndoto yao ya mabadiliko inafikiwa.

Hata hivyo kwa bahati mbaya sana mioyo yao ya mihanga, ushujaa na ujasiri husukumwa na utumwa wa fikra za kimagharibi za kidemokrasia na wakipambania mabadiliko batil nay a ovyo yanayomfanya Allah Taala, Muumba asiwe na nafasi katika maisha yao. Huku ni kutumika vibaya mno Kusikokuwa na mfano!

Ni muhimu ifahamike kuwa uwezo mkubwa wa kufikiri, upeo wa udadisi na tafakuri pana ikiambatana na vipawa vya vijana wetu wa Kiislamu vinapaswa kutumika kwa harakati ya haki na ukweli kwa ajili ya kumridhisha Muumba wet una si vyenginevyo.

Kwa msingi huo, wakati sasa umewadia kwa vijana wa Kiislamu kuunganisha nguvu zao ulimwengu mzima kwa kubeba fikra zitakazoleta mabadiliko halisi ya Kiislamu. Fikra zinazotukomboza na utumwa wa fikra na mfumo batil wa kibepari na usekula na kutupeleka kuwa watumwa na watumishi wa Allah (SW) peke yake. ili kuutawalisha mfumo wa Kiislamu kwa walimwengu wote kwa kupitia dola ya Khilafah inayopaswa kuanzia katika nchi kubwa za Waislamu.

Mhariri

01 Swafar 1448 Hijria

Agosti 2026 M

jukwalakhilafah@gmail.com

wengi wa Bongo Flava kama si wote wamekuwa wakitumia nyimbo zao kuhamasisha maovu katika kijamii, na katika matukio mengi wamejihusisha na matumizi ya dawa za kulevya na ushoga.

Zaidi ya hayo, Bongo Flava si tu chombo cha kuiharibu jamii, bali pia huwajaza vijana matumaini ya uongo na ahadi zisizo za kweli kuhusu maisha bora kupitia utumwa wa kitamaduni.

Kutokana na hali hiyo, vijana wengi huwekeza nguvu, ari na muda wao mwingi katika kuendeleza utamaduni wa kikoloni kwa manufaa ya matajiri wachache wa kibepari wanaomiliki mtandao wa kimataifa wa sekta ya muziki. Kwa hakika, wengi wa wanaoonekana kuwa wasanii wenye mafanikio katika Bongo Flava, kwa mtazamo huu, huwa wamepewa majukumu mengine ya kueneza mmomonyoko wa maadili kama vile ushoga, biashara haramu za madawa ya kulevya nk. Huku wasanii hao wakijificha nyuma ya kichaka cha kuwa wasanii wa muziki.

Uislamu, ukiwa ni mwongozo kamili wa maisha katika nyanja zote, umekataza vitendo vyote vya uovu na upotovu wa maadili kama vile uzinzi, ulevi, ushoga na mengineyo. Chini ya Dola ya Khilafah Rashidah, aina zote za vitendo vya upotovu wa maadili zitapigwa marufuku, na wale wanaovieneza vitendo hivyo au kuhusika, wataadhibiwa kwa ukali ili kulinda jamii, mali na heshima ya mwanadamu.

Imeandikwa na Said Bitomwa

Mjumbe wa Afisi ya Habari Hizb ut Tahrir Tanzania

Kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

Sheria yoyote ikiwemo katiba haiwezekani kamwe kutungwa na watu wengi. Kwa sababu wanaadamu kwa maumbile yao kamwe hawakubaliani. Kwa kuwa kila mmoja ana maslahi anayoyazingatia, wanatofautiana mitazamo, uzoefu na maarifa ya kuyajua mambo na mazingira yaliyowazunguuka. Ndio maana katika mchakato wa katiba wa mwaka 2013 tulimsikia Mwenyekiti wa Tume ya Marekebisho ya katiba Jaji mstaafu Joseph Warioba akitamka wazi bila ya kuficha kwamba katika mchakato ule wa kukusanya maoni ya marekebisho ya katiba, sio maoni yote yatakayochukuliwa kuingizwa katika katiba mpya, bali maoni yatakayozingatiwa ni maoni yanayokubaliana na maslahi ya nchi. Na akasisitiza kwamba wako tayari kufanya “maamuzi magumu”. Suala linakuja nani atatoa tafsiri juu ya dhana ya ‘maslahi ya nchi’. Pia inaonekana kuna walioweka kipimo hicho cha ‘maslahi ya nchi’ kwa tafsiri wanayoionyona wao.

Lakini upande wa pili utaambiwa katika demokrasia huchukuliwa maoni ya wengi. Aidha, utaona mwenye haki ya kutoa hayo yanayoyoitwa maslahi ya nchi ilipaswa kidemokrasia wawe ni wananchi wenyewe. Kwa msingi huu, maana yake mchakato wote wa maoni ya katiba ni mchezo wa kuigiza usiokuwa na uhalisia wala ukweli wowote. Bali ni kuchezea akili za watu Zaidi ya milioni 50 wa Tanzania. Kwa bahati mbaya Waislamu ambao wana muongozo na nuru kutoa kwa Mola wao walipaswa

wawe wa mbele kufedhehi uwongo na udanganyifu wa kati-ba hizi za kibinadamu, lakini baadhi wanashiriki au wanauunda majukwaa ya Waislamu ati kutetea na kushiriki katika mchakato wa kumakinisha ukafiri wa katiba hizi. Wanasahau kwamba unapomakinisha katiba ya kikafiri maana yake unamakinisha ukafiri wote jumla.

2. Katiba ni Milki ya mtu mmoja au kijikundi kidogo cha watu

Katiba za kidemokrasia ambazo wananchi hudai ni zao, kamwe haziwezi kufanya kazi mpaka zitakapopata baraka za kikundi fulani cha watu na sahihi ya raisi. Kwa nini iwe hivyo, ilhali hii ni katiba ya wananchi wenyewe waliyotoa maoni yao? Inamaanisha kwamba maoni yote ya wananchi si chochote si lolote, na katiba humalizikia kuwa ni milki ya mtu mmoja tu. Na hivyo ndivyo ukweli na uhalisia wa utawala wowote ulivyo ambapo baadhi hawaujui au kujisahaulisha ukweli huu. Maumbile ya dhana ya utawala ni suala la kibinafsi na la mtu mmoja tu. Na kamwe haliwezi kuwa suala la wengi, hata kama mtawala mkuu huchukuwa rai za wengine lakini mwisho wa maneno yeye pekee ndie anayekata shauri na si vyenginevya.

Kwa hivyo, kama ni raisi, waziri mkuu au mwengineo kuwa na mamlaka ya kuwa mtu wa mwisho kuipitisha katiba na sheria nyenginezo zote ni dalili kuwa mwisho wa maneno katiba ya kibinaadamu hutegemea mtu mmoja tu, licha ya

Inaendelea Uk 6

MALI ILIYOPORWA

Swali:

Kama inavyojulikana kuwa ardhi ya Palestina yote imeporwa na kijiidola bandia cha Wayahudi. Kuna majengo mengi (real estates) na ardhi nyingi zilizoporwa ambapo wamiliki hasa hawajulikani. Na baadhi ya ardhi hizi dola ya kiyahudi inawamilikisha watu binafsi au makampuni ili kuwekeza humo miradi yao binafsi, nami naishi Palestina nimeelezwa nikodi sehemu kwa ajili ya kufanyia biashara ya majengo (real estate) katika jengo ambalo analimiliki myahudi kwenye ardhi zilizoporwa katika moja ya vitongoji vya Palestina ambapo wenye ardhi hii hawajulikani, ima ni wakimbizi au wamehama.

Je inafaa kukodi ardhi hii? Na ikiwa wenye ardhi hasa hawajulikani, je hukmu inabadilika? Au huchukuliwa (inaamiliwa) ardhi hiyo kuwa ni ardhi iliyoporwa na haifai kuamiliwa kwa kuiuza, kuinunua au kukodi?

Jawabu:

Hakika ya mali iliyoporwa hubakia kuwa ni ya mwenye mali ile, hivyo haifai kuinunua au kuikodi kutoka kwa mporaji.

Ufafanuzi wa hayo ni:

Hakika ya mali iliyoibwa au kuporwa hubakia ni ya mwenye ile mali wa asili popote pale itakapokuwa. Ametoa Ahmad Hadithi kutoka kwa Samura amesema: Kasema Mtume (SAW):

“Kitakapoibiwa kitu kutoka kwa mtu au kikimpotea mtu kitu chake na akakikuta kwenye mikono ya mtu vilevile kilivyo, basi yeye ndie



mwenye haki hasa ya kile kitu. Kisha na arudi mnunuzi kwa muuzaji kwajili (ya kuchukua) thamani (yake)”.

Nass hii ni kuwa mali iliyoibwa ni haki ya mwenye ile mali wa asili. Na pia Mtume (SAW) anasema:” (Dhima ipo)”dhidi ya mkono ulichokichukua (kitu) mpaka ukirejeshe”. Ameitoa Tirmidh na akasema Hadithi ni hasan. Hayo ni kwa mali iliyoporwa.

Kwahiyo, mwenye kupora ardhi ametenda haramu na amechuma dhambi kubwa kwa kauli ya Mtume (SAW):

“Mwenye kudhulumu ardhi kiasi cha shibri tu atazongwa kwa ardhi saba”. Ameitoa Muslim kutoka kwa Hadithi ya Aisha (RA).

Yaani mwenye kupora sehemu yoyote ya ardhi iwe ndogo au kubwa atakua ametenda dhambi kubwa na ataadhibiwa kwayo Akhera. Na hapa duniani atastahiki adhabu ya ta’aziir na atalazimishwa kurejesha alichopora katika hali yake vilevile alivyokipora kwa mwenyewe, kutokana na kauli yake (SAW):

“Dhidi ya mkono ulichokichukua mpaka ukirejeshe”(Tirmidh)

Na kikiharibika katika mikono ya mporaji kile kilichoporwa au akakibadilisha hali yake kama kishona kitambaa kilichoporwa au aliyeyusha madini yalioporwa

au alichinja mnyama aliyeporwa, basi hudhaminiwa thamani yake na mporaji.

Kwahiyo, ukielewa kwamba kitu kimeibiwa au kimeporwa usikinunue na wala usikikodi, na ukiwa (ukihisi) na shubha vilevile usikinunue. Mtume (SAW) anasema: “Wacha lile linalokutia shaka na ulielekee lile lisilokutia shaka”. Ameitoa Tirmidh kutoka kwa Al Hassan bi Ally (RA). Na Tirmidh akasema “Hadithi hii ni hasan na sahihi”

Kwahiyo, muda wa kwamba una yakini kuwa ardhi hiyo imeporwa, ni sawa ukiwa unamfahamu mwenyewe au humfahamu, la muhimu ni kuwa uwe na uhakika kwamba ardhi hiyo imeporwa, itakuwa haifai wewe kuikodi kwa sababu mporaji haimiliki. Na kwa hiyo hawezi kufunga mkataba (‘aqd) wowote na wewe.

Allah akutosheleze na akuepushe na kukodi huko, na tafuta ardhi nyengine ili ukodi, na Allah akubariki kwayo na itakua ni kheri kwako katika dini na dunia. Na Allah yuko pamoja nawe.

Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye Hekima.

Ndugu yenu

Atta Ibn Khalil Abu Al-Rashtah

20, Jamadul akhir 1439H

08/03/2018

Fikra batil ya kikafiri ya kuten-ganisha baina ya dini na siasa (secularism) imeathiri sana katika baadhi ya nyoyo za Waislamu kiasi kwamba mba-ya baadhi yao hawaelewi hata maana ya siasa Kiislamu.

Siasa Kiislamu ni kuyasimamia na kuyachunga mambo ya Umma. Kazi hiyo hutendwa na dola (Khilafah) kwa ku-tumia nguvu zake. Na pia hutendwa na watu binafsi na jumuiya kwa upande wa nasaha.

Katika athari za ufahamu wa kisekula huja na kauli tujiepusheni na kuzungumza siasa, bali tujikite na qadhia kama ndoa na mfano wake. Wakidhani kwamba ndoa ni kitu kando kisichokuwa na fungamano lolote na masuala ya utawala, dola na siasa.

Na baadhi ya mitandao ya Waislamu inapotokea msomaji kutuma mada (post) au kuchangia kuhusiana na masu-ala ya utawala wa Kiislamu na dola yake katika makundi hayo, wasimamizi wa kurasa amma makundi hayo huifuta mada au mchango huo, huku wasimamizi (madmn) huonya kwamba kundi au kurasa yao hiyo haihusiani kabisa na mambo ya kisiasa wakidai ku-wa ni kundi au kurasa ya mambo ya ndoa pekee.

Huku kwa hakika ni kuchang-anyikiwa kwa hali ya juu na kuupa nguvu ukafiri. Amma kwa kujua au kutojua. Vipi utatenganisha baina ya dola na masuala mengine. Ilhali dola



ndio msimamizi wa kisheria katika kila kitu kuanzia uchumi, siasa na masuala ya kijamii ikiwemo ndani yake suala la ndoa.

Mtume SAAW alikuwa Nabii lakini pia alikuwa mtawala, akishi-kilia cheo cha utawala akiwa kiongozi mkuu wa dola, amiri jeshi pia alikuwa qadhi aliyetatua na ku-toa hukmu kwa kulazimisha kwa nguvu kiutekelezaji, na sio ushauri nasaha kama unaotolewa na wanaoitwa maqadhi leo. Alifanya hayo Mtume SAAW katika migo-goro mbali mbali ya ndoa na men-gineyo. Na Waislamu wa zama hizo walimfahamu Mtume SAAW kwa mtazamo sahihi kuwa ni Nabii na mtawala. Ndio maana katika migogoro yao yote walikuwa wanamkabili awatatulie.

Mtume SAAW akiwa qadhi wa Waislamu hakuitenga ndoa kuwa ni kitu kando. Bali akiwa mtawala aliitua migogoro ya ndoa kwa utatuzi wa hukmu thabiti ili kuilin-da taasisi hiyo ambayo kufanikiwa kwake kikweli hulazimu kuwe na dola kuisimamia na kuilinda.

Tukumbuke Mtume SAAW ali-potoa hukmu ya zihar (mume anaemwita mkewe mama yake). kwa mume wa bi Khawlah bint Tha'labah, wakati bibi huyo ali-pomlalamikia Mtume SAAW kwa kusema: *"Mume wangu ametumia utajiri wangu, amestarehe na ujana wangu, na amelichosha tumbo langu kwa kumzalila watoto wengi, sasa nimekuwa mzee siwezi kuzaa*

ananinasabisha kama mama yake."

Mtume SAAW akatoa hukmu ya zihar kama ilivyonukuliwa katika Surat Mujadalah.

Aidha, Mtume SAAW alitua mizozo kadhaa ya wanawake waliozeshwa kwa nguvu (forced marriage) kama ule wa Khansaa binti.

Khudhaam A l-ansaria alipomueleza Mtume SAAW kwamba babake alimuozesha akiwa bikra bila ya idhini yake, nae analichukia jambo hilo. Mtume (SAAW) akavunja ndoa hiyo mara moja.

Kwa upande mwingine, Mtume SAAW aliivunja ndoa ya Abu Rukanah. Wakati mkewe aliposhtaki kwa Mtume SAAW kwamba hamtoshelezi kinyumba.

Kama ilivyonukuliwa katika Sunan ya Abu Daud, kwa mapokezi ya Ibn Abass. *"Ya kwamba Abu Rukanah alimuowa mwanamke wa kabila la Muzinah. Kisha mwanamke huyo akaja kushtaki kwa Mtume SAAW kwa kusema: "Hanitoshelezi hata kwa ukubwa wa unywele huu (huku mwanamke huyo akiashiria unywele uliokuwa mkononi mwake) Kwa hivyo, nitenganishe baina yangu na yeye."* Mtume SAAW akavunja ndoa ile.

Pia, Mtume SAAW alitoa hukmu ya al-khul katika mgogoro wa Habibah bint Sahl, mke wa Thabit ibin Qaays ibn Shammash. Wakati binti huyo aliposema kwa Mtume SAAW: *"Ewe Mjumbe wa Allah sitaki hata kumuona (mume huyu) na lau sio khofu yangu kwa Mwenyezi Mungu ningemtemea mate usoni pake."* Mtume SAAW

Inaendelea uk 8

kuwa wananchi wote huambiwa ati watoe maoni yao. Ajabu ya jambo hili, wanademokrasia hudai katika aqeeda ya mfumo wao kwamba dini iwekwe mbali na mambo ya utawala ili wananchi wenyewe washiriki kujitungia sheria wanazozitaka na kujitawala wenyewe watakavyo, huku wakikataa sheria za Muumba Mmoja wa kila kitu Ambae hana mshirika. Ilhali kumbe sheria wanazojigamba kuwa ni zao hutungwa na mtu mmoja tu, tena ni mwandamu mwenzao kama wao ambae huhisi njaa, maumivu, kulala na hatimae kufa kamwe ! Uduni wa aina gani huu!

3. Viraka vizivyokwisha kwenye katiba.

Kuingizwa katika katiba za kibinadamu viraka viraka kusikokwisha kunadhihirisha mambo matatu makubwa:

Kwanza, kukiri mwanaadamu kumuhitajia Muumba Amuokoe na janga la kushindwa mwanadamu kuweka sheria thabiti za kumtumikia mwanaadamu. Pili, ni dhihirisho kuwa akili ya mwanaadamu ni finyu na ina mipaka. Na tatu, ufinyu wa elimu ya mwanaadamu katika kuyaelewa mambo yake na mazingira kwa jumla kiasi kwamba hadiriki hata kujua jambo linalokuja baada ya muda mfupi hata chini ya sekunde moja. Seuze kujua mambo ya miaka.

Kwa mfano, Katiba ya Marekani iliyotungwa mwaka 1787, kiasi cha kupita miaka minne tu ilipofika mwaka 1791 ikaingizwa viraka kumi ziada (American Politics Today - Maidment & Taipin). Sasa fikiria hiki ni kipindi kifupi mno, na baraza lote la kutunga sheria

halikuweza kuona haja ya kuingiza haki hizo katika mchakato wa utungaji wa awali. Pia, katiba ya India, nchi inayoambiwa ina demokrasia ya hali ya juu katiba yake ina viraka zaidi ya mia moja.

4. Katiba kuandikwa kwa lugha ya kiingereza:

Hii nayo ni dalili kwamba katiba ni ya kigeni ambayo imeletwa kwa raia kwa ajili ya utekelezaji tu. Vipi tena watu wadai kwamba katiba ni yao ilhali hata haiwezi kuandikwa kwa lugha yao. Jambo hilo hudhihirisha mambo kwamba katiba si yao katika lugha, wala si yao hata katika maudhui. Na kwa hakika sio katiba tu, bali takriban sheria zote hubakia katika udhati wake kwa kiingereza. Hii ni kwa sababu nchi zetu haziko huru, kiasi kwamba wakoloni wenye ajenda zao hawaruhusu katiba na sheria kutungwa kwa lugha zisizokuwa zao ili usije ukapatikana mwanya wa kupinda wanachokusudia katika maslahi yao. Aina gani ya unyonge huu! Zaidi ya hayo katiba na sheria zote katika nchi zetu changa hutungwa kwa kutenzwa nguvu kuzingatia sheria zinazoitwa za kimataifa na mawafikiano mbali mbali ya Kimataifa (International Conventions)

5. Kutapatapa kutodumu kwa katiba

Wadau wa katiba za kibinadamu daima wana wasi wasi juu ya kufanikiwa katika utungaji wake, na muda mfupi hudhihirika kutoridhika nayo. Kwa mfano, kama vile alivyowahi kunena raisi wa sasa wa Tanzania kwamba Tanzania itengeneze katiba ambayo angalau itakayodumu kwa miaka 50. Hii maana yake ni kukiri kushindwa kwa katiba za kibinadamu hata kabla ya kumalizika

mchakato wake. Na hilo ni kwa kuwa kuna mambo ambayo hayatogundulikana kipindi hiki itabidi yaje yaingizwe kipindi kijacho. Ikiwa hali ni hiyo, kwa nini basi jukumu la katiba lisiegemezwe kwa Mjuzi wa ghaibu, Anaajua lishalotokea, linalotokea na litakalotokea kwa namna litakavyotokea na ambae pia ni Mjuzi wa kila kilichofichikana.

وَعِنْدَهُ مَفَاتِيحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ وَيَعْلَمُ مَا فِي
الْبَحْرِ وَالْبَحْرِ وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ
فِي ظُلُمَاتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي
كِتَابٍ مُبِينٍ (الأنعام)

"Na ziko katika milki Yake funguo za Ghaibu, hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Anaajua kilichoko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani ila Analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika kitabu kinachobainisha". (TMQ 6: 59)

أَلَّا يَسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي يُخْرِجُ الْخَبَاءَ فِي السَّمَاوَاتِ
وَالْأَرْضِ وَيَعْلَمُ مَا تُخْفُونَ وَمَا تُعْلِنُونَ (النمل):

(25)

"Na (wana nini) hawamsujudii Mwenyezi Mungu ambaye Huyatoa yaliyofichikana katika mbingu na ardhi, na Anayajua mnayoyaficha na mnayoyatangaza" (TMQ 27:25)

6. Hakuna Katiba wala sheria ya kuridhisha makundi yote.

Kusema kwamba katiba za kibinadamu katika nidhamu

Inaendelea Uk 8

KUWAANDAA WANAWAKE KWA DAAWA YA KURUDISHA MAISHA YA KIISLAMU

Kazi ya kurejesha maisha ya Kiislamu kupitia kurejesha dola ya Kiislamu ya Khilafah imechukua manhaji ya Mtume (SAW) ambayo huwahusisha watu wa aina na jinsia zote wanaume na wanawake.



Tukiangalia harakati ya Mtume (SAW) ili wajumuisha wanaume lakini pia wanawake, na wanawake hao waliipa kipaumbele. Aidha wakina mama hao walikuwa ni chachu kwa kuonesha msimamo makini usioyumba katika imani yao pamoja na kuwa liwazo na kuwapa moyo waume zao kwa yale wanayoyapata ya kuudhi na kukatisha tamaa katika daawa.

Mtume mwenyewe (SAW), alikuwa akipata faraja na kutiwa moyo na mkewe Bi Khadija (RA). kila anaporudi nyumbani pale anapopata linaloumiza moyo na kukatisha tamaa katika harakati yake. Kwa mfano, wakati Mtume (SAW) alipopewa wahyi wa kwanza kwenye pango la Jabal Hiraa alifadhaika sana, jambo lililomfanya kukimbilia nyumbani akiwa anatetemeka kwa khofu na woga, lakini baada tu ya kumuhadithia mke wake bibi Khadija bint Khuwelid (RA) alimfariji kwa kumueleza:

"Wewe si mtu wa kuwa na kho-fu. Nina apa kwa Mwenyezi Mungu (SWT), hatokudhalilisha milele. Kwa hakika wewe unaunga udugu na unabeba uzito wa wanyonge, unasaidia masikini, unakirimu wageni, na unasaidia katika matatizo ya

kweli". Mtume (SAW) akapata faraja baada ya kupata maneno hayo na hali yake kurudi ya kawaida.

Na wakati Mtume SAW alipokuwa akielezea wasifu wa mke wake Bibi Khadija (RA) alinukuliwa akisema; "Aliniamini wakati waliponipinga, alinisadikisha wakati waliponikadhibisha, alinishirikisha katika mali yake wakati watu waliponinyima.....".

Bila kusahau msimamo wa mwana-mama shahidi wa mwanzo, Mama Sumayya (RA) na msimamo wa dada yake Umar bin Khataab (RA), yaani Fatma bint Khataab (RA) nk.

Basi katika wanaume kila anayebeba jukumu la kurejesha Khilafah ili kuutawalisha Uislamu katika ardhi ana wajibu wa kuwashirikisha watu wake wa nyumbani katika qadhia hii nyeti. Kwa kuwa kama ilivyokuwa ni wajibu kwa wanaume, basi pia ni wajibu kwa wanawake. Ni jambo la kusikitisha wakati mwingine kuona baadhi ya walinganizi wakiwa na familia zisizokuwa na tofauti na familia zilizoathiriwa na fikra za kimagharibi katika maadili, ufahamu na kuwa kando na dini yao seuze kubeba daawa yake.

Basi kila mlinganizi anapaswa kujua kwamba pamoja na kwamba kwa udhahiri tunaona baadhi katika Ummah unatupinga katika jukumu hili, lakini kihakika unatukubali na kuelewa nafasi yetu katika jamii. Ndio maana wanaharakati na walinganizi wa Khilafah huangaliwa kwa jicho la ziada katika jamii, hata pale

wanapojikwaa au kufanya kitendo fulani kiovu, Umma huja juu kuwasakama kuwa mbona wanalingania Khilafah lakini hawashikamani na Uislamu ipasavyo, ikiwemo ahli na maharimu zao baadhi wakionekana kurandaranda mitaani bila hijabu nk.

Kusemwa hayo na Umma ni hoja inayothibitisha kwamba Umma unawakubali kimaumbile walinganizi, kiasi kwamba hawastahiki kukosea hata kama makosa mengine ya kibinaadamu.

Ni wajibu kwa walinganizi kufahamu kwa kina kuwa ulinganizi wanaobeba ni ujumbe wa ukombozi kwa jinsia zote, basi juhudi za makusudi zinahitajika katika kuwathaqafisha wakina-mama, ahli zetu na maharimu zetu ili nao waweze kuufahamu Uislamu wao na kutambua majukumu yao kuyabeba na kuyatekeleza kikamilifu kwa msukumo wa uchaji Mungu.

Mbinu mbalimbali zinaweza kutumika kufikia huko, zikiwemo kuzungumzia uzuri wa nidhamu za Khilafah katika jamii, uchumi nk. Pia kuonesha ukafiri wa demokrasia na ubaya wa nidhamu yake, kuwabainishia masuluhisho ya Kiislamu katika matatizo yetu hata yaliyomo majumbani mwetu, na kuonesha kwamba hata matatizo tuliyonayo majumbani yamesababishwa na nidhamu inayotutawala. Bila kusahau kuwaalika walinganizi wa kike (mashababati) kwa makusudi majumbani mwetu kwa ajili ya

Inaendelea....uk 8

ya kidemokrasia ni katiba zinazozingatia makundi yote ndani ya jamii, jambo hilo ni muhali na haliwezekani kiuhalisia. Fikra hii ndio iliyomsukumua Waziri wa sheria na utawala bora Mathias Chikawe kuwaeleza mashoga wakiwemo baadhi wa Tanzania walioandamana ndani ya Uswisi alipokuwa ziarani, kwamba ikiwa mashoga hao wanataka haki zao, basi waje wachangie mchakato wa katiba. Jamii za kidemokrasia zina mambo mengi kuanzia ushoga, usagaji, ubasha, ulevi uzinzi nk. Wote hawa wanadai katiba izingatie haki zao. Jambo ambalo kimaumbile ni muhali na haliwezekani. Kwa mfano, ndani ya mwezi wa Aprili mwaka 2013 Bunge la Ufaransa liliidhinisha rasmi ruhusa ya ndoa za jinsia moja ndani ya nchi hiyo. Watu wengi hususan wafuasi wa dini na wanaharakati wa haki za maadili ya kifamilia walipinga vikali suala hilo hadi kuibuka mapambano makali baina yao na polisi. Kwa kuwa suala hilo linaangamiza maadili ya dini na ya kifamilia. Hata hivyo, bunge la nchi hiyo lilipitisha sheria hiyo ambayo ni ushindi kwa mashoga na mabasha, na sio kwa wafuasi wa dini wala watetezi wa maadili ya kifamilia. Kwa hivyo, si kweli kwamba kila kundi litapewa haki yake. Kwa mfano huu, kundi la wanaokubali ndoa hizo ndio waliopata haki na siyo kundi la watu wa maadili ya kifamilia na wafuasi wa dini wanaopinga ndoa za aina hiyo. Kwa hivyo ni uwongo kusema kwamba haki za makundi yote zitazingatiwa ndani

ya katiba hizi.

7. Nyaraka ya kisheria kufanywa na wasio wanasheria.

Katika kituko na kichekesho cha katiba, ni nyaraka ya kisheria ambayo hutungwa na kinachoitwa Bunge la Katiba. Bunge hilo hujiuamisha kinachoitwa wadau kutoka katika makundi mbali mbali lakini wengi sio wanasheria.

Sasa inakuwaje panapokuwa na tatizo la kiafya, suluhisho hutoa wataalamu wa afya, panapokuwa na tatizo la kiusalama suluhisho hutoa watu wa usalama, lakini katika qadhia ya katiba wanaotunga ni Bunge la katiba ambalo sio wanasheria. Hili jambo la ajabu ambalo linapaswa kuzingatiwa na kila mtu makini.

Ndoa...kutoka uk 5

akamuuliza Habibah: *"Jee utamrejeshea shamba lake alilotowa kukupa mahari?"* Habibah akajibu ndio, na alipomrejeshea, Mtume SAAW akawatenganisha. Na zaidi Mtume SAAW alipitisha hukmu ya hadd kwa mwanamke mjane aliyezini kwa kupigwa mawe mwanamke huyo mpaka kufa. Kisa maarufu cha mwanamke wa kabila Ghamid. Kupitishwa hukumu ya hadd kwa aliyeowa au kuolewa pia ni katika kulinda ndoa ili zibakie katika mazingira ya uaminifu, kuepusha uchafu ndani ya jamii na kuhifadhi nasabu sahihi kwa kizazi.

Hivi ndivyo Mtume SAAW alivyokuwa. Kamwe

hakuitenganisha ndoa na dola. Kama ambavyo hakutenganisha mambo mengine ya kiuchumi na kijamii na suala la utawala. Na hivyo pia ndivyo walivyokuwa makhalifah baada yake. Na hivi pia ndivyo itakavyokuwa mara Khilafah ikirudi karibuni kwa idhini ya Allah Taala InshaAllah

Wanawake kutoka uk 7

kuwachangamsha ahli zetu na maharimu zetu kwa ujumla.

Hiyo ndio nafasi ya mwanamke inavyotakiwa iwe kuwa katika ulinganizi, wajumuishwe na sio kutengwa au kuachwa kando. Kwani qadhia tuliyoibeba ni qadhia yetu sote waume na wa kike. Bali pia ni qadhia ya kufa na kupona ambayo mwenye kujifunga nayo kikweli hukadhibishwa, hupata madhila, maudhi, kupigwa, kufungwa, kuuwawa nk.

Sasa tutampata nani wa kutuliwaza, ikiwa hatukuwaandaa ahli zetu na maharimu zetu katika ufahamu bora na kuwaweka tayari katika kubeba majukumu yao ikiwemo kutuvumilia katika maisha hayo yenye mitihani mizito?

Kubwa zaidi tunaondosha dhima kwa Mola wetu na kujiepusha na adhabu kali kwa kuwatelekeza ahli zetu. Kama Allah Taala Alivyotuonya vikali.

"Enyi Mlioamini! Ziokoweni nafsi zenu na watu wenu na moto, ambao kuni zake ni watu na mawe.....". (TMQ 66: 6)